*Swahili Version*

**Level 2**

# DISCIPLESHIP

Day #1 “Understanding and Growing in Our Faith”

**Waebrania 11:1-6**

**1** tBasi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. **2** Maana kwa
hiyo wazee wetu walishuhudiwa. **3** tKwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu,
hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. **4** tKwa imani Habili alimtolea Mungu
dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na
kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena. **5** tKwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala
hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba
amempendeza Mungu. **6** tLakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu
lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Imani ni msingi wa kila jambo maishani. |
| **Andiko** | Waebrania 11:1-6 |
| **Kujisomea Biblia** | Unapomwaza mtu mmoja aliyekuwa na imani kubwa, ni nani anayekuja mawazoni na ni kwa nini?<br>Ni kwa jinsi gani unaweza kuileleza imani?<br>Soma Andiko. Je! Imani imeelezwaje hapo?<br>Ni mifano gani mitatu iliyotolewa katika mistari hii? |
| **Maombi** | “Bwana, nioneshe kama sina au ninayo imani iokoayo.” |
| **Swali/Nukuu** | “Uhakika wa maisha yangu ya milele na Mungu mbinguni haujengwi juu ya yale niyatendayo. Haujengwi juu ya uwezo wangu wa mafanikio katika maisha haya. Si kwamba nikifika mwisho wa maisha yangu na kuona matendo mengi ni mengi kuliko yale mabaya. Hapana, mwisho wetu wa milele umejengwa juu ya kile ambacho Yesu Kristo amekifanya kwa ajili yetu na kwamba tumeupokea msamaha wake kwa ajili ya dhambi zetu.” Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 11. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Kama huzijui sana habari za Kaini, Habili, na Henoko, zisome katika Mwanzo sura ya 4 na 5. |

**Mathayo 8:5-13**

**5** ttHata alipoingia Kapernaumu, akida mmoja alimjia, **6** akamsihi, akisema, Bwana, mtumishi wangu amelala
nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana. **7** Yesu akamwambia, Nitakuja, nimponye. **8** Yule akida
akamjibu, akasema, Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi
wangu atapona. **9** Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu;
nikimwambia huyu, Nenda, huenda; na huyu, Njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya. **10** tYesu
aliposikia hayo, alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, Amin, nawaambieni, Sijaona imani kubwa namna
hii, kwa ye yote katika Israeli. **11** tNami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na
magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni; **12** tbali wana
wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. **13** tNaye Yesu akamwambia
yule akida, Nenda zako; na iwe kwako kama ulivyoamini. Mtumishi wake akapona saa ile ile.

**Mathayo 8:23-27**

**23** ttAkapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata. **24** Kukawa msukosuko mkuu baharini, hata chombo
kikafunikizwa na mawimbi; naye alikuwa amelala usingizi. **25** Wanafunzi wake wakamwendea,
wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia. **26** tAkawaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa
imani haba? Mara akaondoka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu. **27** Wale watu wakamaka
wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii?

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Imani yetu inapaswa kuendelea kukua. |
| **Andiko** | Mathayo 8:5-13; 23-27 |
| **Kujisomea Biblia** | Unagundua nini juu ya maafisa wa jeshi la Kirumi?<br>Kwa nini Yesu alimwambia kuwa alikuwa na imani kubwa namna hii?<br>Kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi kuwa walikuwa na imani haba? (mistari 23-26)<br>Wote, Akida na wanafunzi wa Yesu walikuwa na imani. Lakini tofauti yao ilikuwa ni nini?<br>Je! Usingewaza kwamba wale watu waliotembea na Yesu wangekuwa na imani kubwa kuliko yule mtu ambaye amekutana na Yesu tu? Hii inawezekanaje? |
| **Maombi** | "Bwana, kuza imani yangu. Usiniruhusu nikuchukue wewe kwa mzaha au kuridhika katika kukua kwangu kiroho." |
| **Swali/Nukuu** | "Wakristo wengi…wanahangaika na maisha, wakijitahidi kutengeneza njia zao maishani, wakijaribu kuyaelekeza maisha yao katika kile ambacho wanadhani ni hatima yao. Kile ambacho hawagundui ni kwamba Mungu anavyo vingi kwa ajili yao kuliko uzoefu wao walio nao sasa. Wanaweza kuonekana wanakua kwa hatua…lakini hawajihusishi kikamilifu na mambo ya Ufalme wa Mungu." Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 12. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Orodhesha jambo moja tu ambalo unaweza kulifanya leo ili kuanza kuikuza imani yako—kisha fanya! |

*Swahili Version*

**Level 2**

# DISCIPLESHIP

Day #2 “Deepening Our Relationship With God”

**Zaburi 24:3-10**

**3** Ni nani atakayepanda katika mlima wa BWANA? Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake? **4** tMtu
aliye na mikono safi na moyo mweupe, Asiyeiinua nafsi yake kwa ubatili, Wala hakuapa kwa hila. **5** Atapokea
baraka kwa BWANA, Na haki kwa Mungu wa wokovu wake. **6** Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao,
Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa Yakobo. **7** tInueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango
ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia. **8** Ni nani Mfalme wa utukufu? BWANA mwenye nguvu, hodari,
BWANA hodari wa vita. **9** Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naam, viinueni, enyi malango ya milele,
Mfalme wa utukufu apate kuingia. **10** Ni nani huyu Mfalme wa utukufu? BWANA wa majeshi, Yeye ndiye
Mfalme wa utukufu.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Mungu anatamani mahusiano ya karibu sana nasi lakini kuna vipingamizi ambavyo hujitokeza njiani |
| **Andiko** | Zaburi 24:3-10 |
| **Kujisomea Biblia** | Katika mstari wa 4 ni mambo gani manne yametajwa yanayotakiwa katika kumkaribia Mungu?<br>Ni baadhi ya miungu ipi maishani mwetu ambayo tunaiinua badala ya Mungu?<br>Kuna ahadi gani kwa wale wamtafutao Mungu kwa haki? (mstari 5)<br>Mistari ya 7-10 inatumia ulinganifu wa mji unaofungua malango yake ili kumkaribisha mfalme anayerudi kwa ushindi kutoka vitani. Je! Kuna “malango” yo yote au vikwazo vyo vyote maishani mwako ambavyo humfanya Mungu asiinuliwe maishani mwako? |
| **Maombi** | “Bwana, ninaomba kwamba matendo yangu, upengo wangu, na kujali kwangu vikupendeze wewe. Nisaidie kung’aa na kusema iliyo kweli. Nioneshe kama kuna vikwazo vyo vyote vinavyozuia mahusiano yetu na kukuzuia kuonesha utukufu wako kupitia mimi.” |
| **Swali/Nukuu** | “Tunapoingia dhambini, kufikiri kwetu husongwa sana. Tunaanza kupoteza hisia za mwongozo wa maadili mema kadri tunavyomzimisha Roho Mtakatifu. Ni sawa sawa na kutembea porini uskuku wa giza, lazima tu utapotea njia.” Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 104. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Kama katika kipengele cha Kujisomea biblia uliogundua vikwazo vyo vyote vile, basi viorodheshe. Kisha, kwa hali ya maombi amua ni hatua gani utaanza kuchukua leo ili kuviondoa vipingamizi hivyo. |

# Level 2
# DISCIPLESHIP



**Zaburi 119:1-16**

1 Heri walio kamili njia zao, Waendao katika sheria ya Bwana. 2 Heri wazitiio shuhuda zake, Wamtafutao kwa
moyo wote. 3 Naam, hawakutenda ubatili, Wamekwenda katika njia zake. 4 Wewe umetuamuru mausia yako,
Ili sisi tuyatii sana. 5 Ningependa njia zangu ziwe thabiti, Nizitii amri zako. 6 Ndipo mimi sitaaibika,
Nikiyaangalia maagizo yako yote. 7 Nitakushukuru kwa unyofu wa moyo, Nikiisha kujifunza hukumu za haki
yako 8 Nitazitii amri zako, Usiniache kabisa 9 Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno
lako. 10 Kwa moyo wangu wote nimekutafuta, Usiniache nipotee mbali na maagizo yako. 11 Moyoni mwangu
nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi. 12 Ee Bwana, umehimidiwa, Unifundishe amri zako.
13 Kwa midomo yangu nimezisimulia Hukumu zote za kinywa chako. 14 Nimeifurahia njia ya shuhuda zako
Kana kwamba ni mali mengi. 15 Nitayatafakari mausia yako, Nami nitaziangalia njia zako. 16 Nitajifurahisha
sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Neno la Mungu ni la muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. |
| **Andiko** | Zaburi 119:1-16 |
| **Kujisomea Biblia** | Tunajifunza nini juu ya Mungu katika Biblia ambacho hatuwezi kujifunza mahali pengine po pote pale? (mstari 4)<br>Neno la Mungu lina matokeo gani katika mahusiano yetu na Mungu? (mstari 7)<br>Kuna siri gani ya kuishi maisha ya utauwa? (mstari 9)<br>Ina maana gani kuliweka neno la Mungu moyoni mwako na ni faida gani inayopatikana? (mstari 11) |
| **Maombi** | "Mungu, nisaidie kukua katika pendo langu, kulijua na kulikubali. Nisaidie kulipa kipaumbele ili niweze kupata muda wa kulisoma kila wakati na kila siku." |
| **Swali/Nukuu** | "Kaa katika Neno. Kuna usemi wa zamani usemao, 'Biblia itakutenga na dhambi na dhambi itakutenda na Biblia'…Neno la Mungu litatumulikia kati ya wema na ubaya. Neno la Mungu litatuepusha na hali ya kuanguka majaribuni." Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 104. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Kariri Zaburi 119:11 |

*Swahili Version*

Level 2
**DISCIPLESHIP**

Day #3 "The Christian Life is a Journey"

**Wafilipi 2:12-13**

**12** tBasi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana
mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. **13** tKwa maana ndiye
Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Ninapaswa kujali ukuaji wa maisha yangu ya kiroho |
| **Andiko** | Wafilipi 2:12-13 |
| **Kujisomea Biblia** | Ni safari gani iliyokuvutia sana ambayo umewahi kusafiri?<br>Ni kwa jinsi gani maisha ya Kikristo ni kama safari?<br>Paulo, akisema na waamini, anasema kwamba "tuutimize" wokovu wetu. Je! Hii inatofauti gani na "kujitahidi" kwa ajili ya wokovu wetu. Je! Tuwe na nia gani tunapoutimiza wokovu wetu? (mstari 13)<br>Mungu ana kazi gani katika safari yetu ya kuutimiza wokovu wetu? |
| **Maombi** | "Mungu, ninakushukuru siku ya leo kwa kuwa wewe unatenda kazi maishani mwangu ili kuruhusu mapenzi na matendo yangu kukubaliana na matakwa yako kwa ajili ya maisha yangu. Tafashali, nipe hali ya kutambua umuhimu wa kuyaona maisha yangu ya kiroho yanakua kama." |
| **Swali/Nukuu** | "Maendeleo binafsi ya kiroho ni jambo la kupewa umuhimu mkubwa, na jambo ambalo halitokea kwa bahati mbaya. Ni lazima ulifanyie kazi." Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 28. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Kariri Wafilipi 2:12-13 |

**1 Wakorintho 3:10-15**

**10** tKwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka
msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. **11** tMaana
msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo. **12**
Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au
manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. **13** tMaana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto;
na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. **14** Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa,
atapata thawabu. **15** Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama
kwa moto.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Tunapaswa kutaambua na kuchuchumilia yale yenye maana zaidi maishani, mambo ambayo yatadumu zaidi ya maisha haya |
| **Andiko** | 1 Wakorintho 3:10-15 |
| **Kujisomea Biblia** | Ni kielelezo gani Mtume Paulo anakitumia kuonesha maisha ya Kikristo? (mistari 10-11)<br>Tunauamuzi gani inapofikia hatua ya “vifaa vya ujenzi”? (mistari 12-13)<br>Ni mambo gani maishani tunayoweza kuyafanya lakini yasipite katika kipimo cha Mungu?<br>Zingatia kwamba mistari 14-15 inazungumzia thawabu na sio kupata uzima uzima wa milele. Mtu afanye nini ili kupata uzima wa milele? |
| **Maombi** | “Mungu nisaidie kuitafuta ile dhababu kubwa maishani mwangu—mambo yale yanayokuletea heshima na yatadumu milele.” |
| **Swali/Nukuu** | “Kuitafuta dhahabu iliyo kubwa ni ujumbe wenye nguvu sana kwamba maisha ni zaidi ya medali za dhahabu au kazi nzuri yenye mafao mazuri. Dhahabu hii kubwa inapatikana katika maisha yaliyo ndani ya Kristo tu.” Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 119. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Chukua karatasi. Kushoto mwa karatasi hiyo andika “miti.” Kulia andika “gdahabu kubwa.” Sasa chini ya kila moja orodhesha mambo 3-5 ambayo yataoana na kila kategoria hiyo hapo juu. Ukiipitia orodha yako hiyo orodhesha (vipengele vingine 6-10) sasa hivi. Hivyo, weka namba “1” kwene kipengele ambacho kinachukua asilimia nyingi ya usikivu wako, shauku, na rasilimali (muda, pesa, n.k.) kisha “2” kwa lile ambalo unadhani linafuatia na kuendelea. Kisha ipitie orodha hiyo ili uone maisha yako yanasisitiza “miti, majani, au manyasi” au dhahabu. Ni mabadiliko gani unayotakiwa uyafanye ili uipate ile dhahabu? |

*Swahili Version*

**Level 2**

# DISCIPLESHIP

Day #4 “Spiritual Warfare”

**Waefeso 6:10-18**

**10** tHatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. **11** tVaeni silaha zote za
Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. **12** tKwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na
nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika
ulimwengu wa roho. **13** tKwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya
uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. **14** tBasi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii
ya haki kifuani, **15** tna kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; **16** tzaidi ya yote mkiitwaa ngao
ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. **17** tTena ipokeeni
chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; **18** tkwa sala zote na maombi mkisali kila
wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Tunapaswa kujiandaa vema kwa ajili ya vita vya kiroho tutakavyokumbana navyo. |
| **Andiko** | Waefeso 6:10-18 |
| **Kujisomea Biblia** | Ni kwa jinsi gani tunaweza kusimama dhidi ya mishale ya Shetani maishani mwetu? (mistari 10-11)<br>Ni nini kinachoendelea karibu nasi lakini hatuwezi kukiona? (mstari 12)<br>Orodhesha vile vipande sita ambavyo vinavyoiunda “silaha” ya Mungu? (mistari 14-17)<br>Mbali na matumizi ya silaha yetu, tunaweza kufanya nini zaidi? (mstari 18) |
| **Maombi** | “Mungu, nisaidie kusimama kwa nguvu yako mbele ya uovu na mbinu za kipepo ambazo zinaniwinda kuniangusha. Nioneshe ni wapi niko wazi kwa ajili ya yule mwovu, nitie nguvu niweze kuzitumia zile zana ambazo umenipa.” |
| **Swali/Nukuu** | “Ili mradi kuna dhambi ulimwenguni, daima kutakuwa na jamii ya kipagani iliyo tayari kutuondosha kabisa. Ili mradi kuna watu bila Kristo, kutakuwa na mvuto mkubwa wa kumwacha Bwana…Habari njema ni hii sisi tu washindi…tunaweza kuogelea dhidi ya mto huo.” Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 111. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Zile zana sita zinazounda silaha ya Mungu, jitambue wewe mwenyewe ni katika eneo gani una udhaifu nalo. Je! Unajua kuzitumia zana hizo ulizopewa? Baadaye, mwombe Mungu akuoneshe yale unayoweza kuanza kuyafanya leo hii ili kuliimarisha eneo hili—kisha fanya. |

**2 Wakorintho 4:7-18**
**7** tLakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka
kwetu. **8** tPande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; **9** twaudhiwa, bali
hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; **10** tsiku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili
uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. **11** tKwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa
ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti. **12** Basi hapo mauti
hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. **13** tLakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama
ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena; **14**
ttukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha
pamoja nanyi. **15** tKwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio
wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe. **16** tKwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje
unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. **17** tMaana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya
muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; **18** ttusiviangalie
vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya
milele.

| | |
|---|---|
| **Wazo** | Mahangaiko ni sehemu ya maisha. Lakini kuna kanuni za kibiblia ambazo tunaweza kuzifuata ili kushinda wakati wa mahangaiko yetu. |
| **Andiko** | 2 Wakorintho 4:7-18 |
| **Kujisomea Biblia** | Ni baadhi ya mambo gani maishani yanayoweza kuleta hali ya kuhangaika au msukumo ndani yetu?<br>Ni hali zipi nne Paulo anazieleza katika mistari ya 8-9?<br>Ingawa hali hizi nne ni ngumu hazipaswi kuwa ni za uharibifu. Ni tumaini gani analitoa kwa kila moja?<br>Kwa nini Mungu anaturuhusu tupite katika misukosuko ya maisha? (mistari 10-12)<br>Ni siri gani ya kutuwezesha kuendelea mbele wakati wa mahangaiko? (mistari 16-18) |
| **Maombi** | “Bwana nisaidie nikuelekezee wewe macho yangu na kupumzika katika uhakika wa pendo na ulinzi wako. Nikumbushe kwamba yale yote ninayoyaendea kwa sasa ni ya muda tu.” |
| **Swali/Nukuu** | “Ukitazama kwa haraka, utadhani kwamba Mungu alikuwa amemwacha Yusufu. Amemtumikia Mungu na Potifa kwa uadilifu, lakini inaonekana Mungu ‘amemtelekeza afe peke yake’…Sawa, lakini Yusufu hakuwaza hivyo. Yeye aliendelea kuishi kwa ajili ya Bwana kama alivyofanya siku zote. Yawezekana hali yake ilikuwa imebadilika lakini shauku yake kwa Mungu ilikuwa palepale.” Frank Banfill, *Maxpoint*, ukurasa 72. |
| **Hatua kwa Vitendo** | Andika lile tatizo kubwa kabisa linalikusumbua sasa hivi. Orodhesha mambo 2-3 yaliyosababisha tatizo hilo. Una mawazo gani katika kuzishughulikia sababu hizi zilizolisababisha tatizo hilo? Je! Kuna njia ya kivitendo ambayo unaweza kuifanya unaposhughulika na sababu hizo? Omba sasa na mwulize Mungu akupe hekima. Si kila tatizo lazima lipate suluhu, lakini mengi yanaweza kama tutaishughulikia mizizi yake na kuitafuta hekima ya Mungu ili kupata mpango kamili wa kulishughulikia tatizo. |